

**Maafikiano ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika 2003**  
**Convention for the Safeguarding of the Intangible Cultural Heritage**

**Translated by the Panel of Kiswahili experts convened by  
the Department of Culture, Ministry of State for National Heritage and Culture,  
Republic of Kenya**

**26 October 2008, Nairobi**

## **Maafikiano ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika 2003**

Paris, 17 Oktoba 2003

Kongamano Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni ambalo kwingineko katika makala hii linarejelewa kama UNESCO, linalokutana jijini Paris – Ufaransa, kuanzia terehe 29 Septemba mpaka tarehe 17, Oktoba 2003, katika kikao chake cha 32,

Kwa kurejelea vyombo vilivyopo vya kimataifa kuhusu haki za kibinadamu, hususan, kwa Azimio la Pamoja la Haki za Kibinadamu la mwaka wa 1948, Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Uchumi, Jamii na Haki za Kitamaduni ya mwaka wa 1966, na Makubaliano ya Kimataifa ya Haki za Kijamii na Kisiasa ya mwaka wa 1966,

Kwa kuzingatia umuhimu wa turathi za tamaduni zisizogusika kama nyenzo na kiini cha kusambaa kwa tamaduni na hakikisho la maendeleo endelevu, kama ilivyosisitizwa kwenye Mapendekezo ya UNESCO kuhusu Ulinzi wa Tamaduni za Kiasili na Elimu kuhusu Mila na Desturi za Kijamii ya mwaka wa 1989, kwenye Makubaliano ya Pamoja kuhusu uanuwai kwa Tamaduni ya mwaka wa 2001, na katika Azimio la Istanbul la mwaka wa 2002 lililopitishwa na Jopo la kikao cha tatu cha Mawaziri wa Tamaduni,

Kuzingatia utegemeano mkubwa uliopo kati ya turathi za tamaduni zisizogusika, tamaduni-gusika, na turathi asili,

Kwa kufahamu kwamba taratibu za kiutandawazi na mabadiliko ya kijamii, pamoja na hali zinazotokana na mambo hayo, huwezesha uhusiano mpya unaojitokeza kati ya jamii, kadhalika husababisha hali za wanadamu kutostahimiliana, tishio la kudidimiza, kupoteza na kuharibu kabisa turathi za tamaduni zisizogusika, hususan, kutokana na kutokuwepo kwa rasilimali muhimu za kulinda turathi hizo,

Kwa kuyaelewa makubaliano ya pamoja na kufuatia hisia za wengi katika kuulinda turathi ya tamaduni zisizogusika za wanadamu,

Kwa kufahamu kwamba jamii, hususan jamii za kiasili, vikundi, wakati mwingine, watu binafsi hutekeleza majukumu muhimu ya uzalishaji, ulinzi, uendelezaji na uzalishaji-upya wa turathi za tamaduni zisizogusika, na hivyo, kusaidia kurutubisha uanuwai wa tamaduni na ubunifu wa binadamu,

Kwa kutambua mchango mkubwa wa shughuli za UNESCO katika uundaji wa vyombo vya kulinda taratibu za turathi za kijamii, hususan Maafikiano ya Ulindaji wa Turathi za Kilimwengu za Kitamaduni na Kiasili ya mwaka wa 1972,

Kwa kutambua zaidi kwamba hadi sasa hakuna chombo cha kimataifa cha maafikiano kinacholinda turathi za tamaduni zisizogusika,

Kwa kuzingatia kwamba makubaliano ya kimataifa, mapendekezo na maamuzi yaliyopo kuhusiana na turathi za kitamaduni na kiasili, yanahitaji kuimarishwa na kujalizwa kwa kuundiwa vifungu vipya vinavyohusiana na turathi za tamaduni zisizogusika,

Kwa kuzingatia haja ya utambuzi mkubwa zaidi kwa mapendekezo hayo, hususan miongoni mwa vijana wa vizazi vichanga, kuhusu umuhimu wa turathi za tamaduni zisizogusika na ulinzi wake,

Kwa kuzingatia kwamba jamii ya kimataifa inafaa kuchangia, pamoja na Mataifa Wanachama katika Maafikiano hayo, kuhusu kulindwa kwa turathi kama hizo, kwa moyo wa ushirikiano na kusaidiana,

Kwa kutafakari kuhusu miradi ya UNESCO inayohusiana na turathi za tamaduni zisizogusika, hususan Tangazo la Vito vya Masimulizi na Turathi Zisizogusika za Wanadamu,

Kwa kuzingatia wajibu mkubwa wa turathi za tamaduni zisizogusika kama msingi wa kuwaleta pamoja wanadamu kwa kuwatangamanisha na kuhakikisha ubadilishanaji na maelewano kati yao,

Linayapitisha Makubaliano haya katika siku hii ya tarehe 17, Oktoba 2003.

## I. Kanuni za Jumla

### Kifungu cha 1– Lengo la Kongamano

Malengo kamili ya Muafaka huu:

- (a) Kulinda turathi za tamaduni zisizogusika;
- (b) Kuhakikisha kwamba turathi za tamaduni zisizogusika za wanajamii, vikundi husika na watu binafsi wanaohusika zimeheshimiwa;
- (c) Kuimarisha utambuzi katika viwango vya kiwilaya, kitaifa na kimataifa kuhusiana na umuhimu wa turathi za tamaduni zisizogusika, na hatimaye kuhakikisha kwamba kuna kuthaminiana;
- (d) Kutoa fursa ya usaidizi na ushirikiano wa kimataifa.

### Kifungu cha 2 – Fafanuzi

Kwa minajili ya Maafikano hayo,

1. “Turathi za Tamaduni zisizogusika” inamaanisha desturi, viwakilishwaji, mwonekano, maarifa, ujuzi – zikiwepo ala, vitu vya kuundwa, vito na kuheshimu mipaka yoyote ya kitamaduni inayohusishwa na mambo hayo – jamii, vikundi na, wakati mwingine, watu kuvitambua kama sehemu mojawapo ya turathi za kitamaduni. Turathi hizi za Tamaduni Zisizogusika, zilizopokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, aghalabu hubuniwa na jamii na vikundi, kulingana na mazingira yao, uingiliano wao na uasili pamoja na historia yao, na kuwapa hali ya kutambulika na kuendelea kuwepo, na hivyo basi kuikuza nidhamu ya uanuwai wa tamaduni na ubunifu wa kibinadamu. Kwa madhumuni ya Maafikiano haya, suala la turathi za tamaduni zisizogusika litapewa kipaumbele kulingana na vyombo vilivyopo vya kimataifa vinavyozingatia haki za kibinadamu, na hali kadhalika kulingana na kuheshimiana kwa jamii, vikundi na watu binafsi, na wa maendeleo endelevu.

2. “Turathi za tamaduni zisizogusika”, kama ilivyofafanuliwa katika aya ya 1 hapo juu, imedhihirishwa katika nyanja zifuatazo miongoni mwa nyingine:

- (a) Mila za kimazungumzo na mwoneko, ikiwa ni pamoja na lugha kama chombo cha turathi za tamaduni zisizogusika ;
- (b) Sanaa za maigizo;
- (c) Desturi za kijamii, matambiko na matukio ya kusherehekea;
- (d) Maarifa ya kijamii kuhusiana na asili na ulimwengu;
- (e) Ufundistadi wa kiasili.

3. “Kulinda” inamaanisha hatua zilizokusudiwa ili kuhakikisha ufaafu au kutimilika kwa turathi za tamaduni zisizogusika, ikiwa ni pamoja na utambulisho, uhifadhi wa nyaraka, utafiti, utunzaji, ulinzi, utangazaji, uboreshaji, usambazaji, hususan kupitia mbinu za elimu rasmi na isiyo rasmi, na hali kadhalika ufufuaji wa vipengee mbali mbali vya turathi kama hizo.

4. “Mataifa Wanachama” humaanisha Mataifa yaliyofungamanishwa na Maafikiano haya na ambapo Maafikiano haya yanatekelezwa.

5. Maafikiano haya yatatumika kama yalivyo katika maeneo yaliyorejelewa katika kifungu cha 33, ambayo yatayazingatia Maafikiano haya kwa mujibu wa kanuni zilizofanuliwa katika kifungu hicho. Kwa misingi hiyo, maelezo haya ya “Mataifa Wanachama” pia hurejelea maeneo kama hayo.

### **Kifungu cha 3 – Uhusiano na vyombo vinginevyo vya kimataifa**

Katika maafikiano haya, hakuna kinachofaa kufasiriwa kama:

(a) Kubadilisha hadhi au kupunguza kiwango cha ulinzi chini ya Maafikiano ya 1972 kuhusu Ulinzi wa Utamaduni na Uasili wa Turathi za Kilimwengu, wa Amali za Turathi za Kidunia ambayo yanahusiana na sehemu moja ya turathi za tamaduni zisizogusika inahusishwa moja kwa moja; ama

(b) Kuathiri haki na majukumu ya Mataifa Wanachama kutokana na vyombo vya kimataifa vinavyohusiana na haki miliki za uwezo wa kiakili ama kwa matumizi ya rasilimali za elimu-viumbe na kiekolojia ambazo wana uhusiano nazo.

## **II. Viungo vya Maafikiano**

### **Kifungu cha 4 – Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama**

1. Mkutano Mkuu wa Mataifa Wanachama umeanzishwa, utakaofahamika kama “Mkutano Mkuu”. Mkutano Mkuu ndio chombo kikuu chenye mamlaka cha Maafikiano haya.

2. Mkutano Mkuu utaitishwa katika vikao vya kawaida baada ya kila miaka miwili. Vikao vinaweza kufanyika kwa hali isiyo ya kawaida kila inapobidi ama kwa ombi la Kamati ya Muungano kati ya Serikali ili kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika au pengine hata thuluthi moja ya Mataifa Wanachama.

3. Mkutano Mkuu utapitisha Masharti yake ya Utendakazi.

### **Kifungu cha 5 – Kamati ya Muungano kati ya Serikali kuhusu Ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika**

1. Kamati ya Muungano kati ya Serikali ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika, itakayofahamika kama “Kamati”, imeundwa na UNESCO. Itahusisha wawakilishi 18 wa Mataifa Wanachama, waliochaguliwa kwenye mkutano wa Baraza Kuu, baada ya Maafikiano haya kupitishwa kulingana na Kifungu cha Kanuni ya 34.

2. Idadi ya Wanachama wa Mataifa yaliyo kwenye Kamati itaongezwa hadi 24 pindi tu idadi ya Mataifa Wanachama wa Maafikiano hayo itakapofikia 50.

#### **Kifungu cha 6 – Uchaguzi na Kipindi cha Majukumu ya Kamati ya Wanachama wa Mataifa husika**

1. Uchaguzi wa Kamati ya Wanachama wa Mataifa husika utayaheshimu kikamilifu masharti yanayozingatia usawa wa kiuwakilishi kwenye misingi ya kijiografia na kizamu.
2. Kamati ya Wanachama wa Mataifa husika itachaguliwa kwa kipindi cha miaka minne na Mataifa Wanachama ili kuhudhuria kwenye Maafikiano ya Mkutano Mkuu.
3. Hata hivyo, kipindi cha majukumu ya ofisi, cha nusu ya Wanachama wa kamati ya Mataifa husika waliochaguliwa kwenye uchaguzi wa kwanza, watahudumu kwa muda wa miaka miwili pekee. Mataifa hayo yatateuliwa kinasibu katika uchaguzi wa kwanza.
4. Kila miaka miwili, Kongamano la Mkutano Mkuu litaongeza muda wa nusu ya Wanachama wa Kamati ya Mataifa husika.
5. Kadhalika Kongamano hilo litachagua wanachama wengi wa kamati ya Mataifa husika ili kujaliza nafasi zilizobakia.
6. Taifa Mwanachama la Kamati, huenda lisichaguliwe kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo.
7. Mataifa Wanachama wa Kamati yatachagua wawakilishi wao walio na ujuzi wa kutosha katika nyanja mbali mbali kwenye turathi za tamaduni zisizogusika.

#### **Kifungu cha 7 – Majukumu ya Kamati**

Bila ya kupendelea au kuuchujua uwezo uliopewa kamati na Maafikiano haya, majukumu ya Kamati hii yatakuwa:

- (a) Kuyatangaza malengo ya Maafikiano hayo, kuhimiza na kusimamia utekelezwaji wake;
- (b) Kutoa miongozo kuhusu mbinu bora za utendaji kazi na kuweka wazi mapendekezo ya kulinda turathi za tamaduni zisizogusika;
- (c) Kutayarisha na kuwasilisha rasimu kwenye Mkutano Mkuu ili kuidhinishwa kwa mpango ili kutumiwa kwenye rasilimali za Hazina, kulingana na kifungu cha 25;
- (d) Kutafuta mbinu za kuongeza rasilimali yake, na kuhakikisha kwamba hilo linatendeka kulingana na kifungu cha 25;
- (e) Kutayarisha na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu ili kuidhinishwa mielekeo ya usimamizi inayohusiana na utekelezaji wa Maafikiano;
- (f) Kuchunguza ripoti zilizotolewa na Mataifa Wanachama, na kuzifanyia muhtasari kwa minajili ya Mkutano Mkuu kulingana na kifungu cha 29;

(g) Kuchunguza maombi yaliyotumwa na Mataifa Wanachama, kisha kutoa maamuzi kulingana na vigezo bora vya uchaguaji vilivyozishwa na Kamati na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu kwa:

- (i) Maandishi yaliyopo kwenye orodha na mapendekezo yaliyotajwa chini ya Kifungu cha 16, 17, na 18;
- (ii) Kuruhusu usaidizi wa kimataifa kulingana na Kifungu cha 22.

### **Kifungu cha 8 – Mbinu za Utendakazi wa Kamati**

1. Kamati itajiwajibisha na kuripoti shughuli na maamuzi yake yote kwa Mkutano Mkuu.
2. Kamati itafuata Utaratibu wa Masharti yake kwa wingi wa thuluthi mbili ya wanachama wake.
3. Kamati inaweza kuunda, kwa kipindi kifupi, na kwa maamuzi yake, mashirika yoyote yatakayoendesha shughuli zake kiushauri.
4. Kamati hiyo inaweza kualika kwenye mikutano yake wawakilishi wa mashirika ya kibinafsi au la umma, au pia watu binafsi walio na umilisi unaotambulika katika nyanja mbali mbali za turathi za tamaduni zisizogusika, ili kushauriana nao kuhusu masuala tofauti tofauti.

### **Kifungu cha 9 – Utambulisho Rasmi wa Mashirika ya Ushauri**

1. Kamati hiyo itapendekeza kwa Mkutano Mkuu, kuyatambulisha rasmi mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyo na umilisi wa shughuli zinazohusu turathi za tamaduni zisizogusika kuwa kama washauri wa kamati.
2. Kamati hiyo pia itapendekeza kwa Mkutano Mkuu vile vigezo na mifumo inayofaa kutumika katika utambulisho huo rasmi.

### **Kifungu cha 10 – Afisi ya Utawala**

1. Kamati hiyo itasaidiwa na Afisi ya Utawala ya UNESCO.
2. Afisi hiyo ya Utawala itatayarisha nyaraka za Mkutano Mkuu na kwa Kamati, na kadhalika kutayarisha ajenda ya rasimu ya mkutano, mbali na kuhakikisha utekelezwaji wa maamuzi yake.

## **III. Kulinda turathi za tamaduni zisizogusika katika kiwango cha kitaifa**

### **Kifungu cha 11 – Majukumu ya Mataifa Wanachama**

Kila Taifa Mwanachama:

- (a) Litachukua hatua zifaazo ili kuhakikisha kwamba turathi za tamaduni zisizogusika zimelindwa kikamilifu katika eneo lake;

(b) Litazingatia kwamba kati ya hatua muhimu za ulinzi huo uliotajwa kwenye kifungu cha 2, aya ya 3, litazifahamu na kufafanua vipengele vinavyohusiana na turathi za tamaduni zisizogusika zilizopo katika eneo lake, kwa kuwahusisha wanajamii, vikundi na mashirika faafu yasiyo ya kiserikali.

### **Kifungu cha 12 – Orodha ya Turathi Zisizogusika**

1. Kila Taifa Mwanachama litahakikisha kutambuliwa kwa lengo la kulinda turathi za tamaduni zisizogusika zilizo kwenye orodha moja au zaidi katika eneo lake, kulingana na hali yake. Orodha hizi zitarekebishwa mara kwa mara.
2. Kulingana na kifungu 29, kila Taifa Mwanachama litawasilisha ripoti yake kwa Kamati, ili kutoa taarifa muhimu kuhusu orodha hizo.

### **Kifungu cha 13 – Taratibu zingine za Ulinzi**

Ili kuhakikisha ulinzi, maendeleo na utangazaji wa turathi za tamaduni zisizogusika zilizoko katika eneo lake, kila Taifa Mwanachama litajitahidi kutekeleza yafuatayo:

- (a) Kufuata sera ya jumla inayolenga kutangaza majukumu ya turathi za tamaduni zisizogusika kwenye jamii, na katika kuzihusisha taratibu za kulinda turathi kama hizo katika miradi ya mipango;
- (b) Kuanzisha shirika moja au zaidi lenye umilisi wa kulinda turathi hizo za tamaduni zisizogusika katika eneo lake;
- (c) Kuendeleza mafunzo ya kisayansi, kiteknolojia na kisanaa, na hali kadhalika, mifumo ya kiutafiti kwa lengo la kulinda vyema turathi za tamaduni zisizogusika, hususan, zile zilizo hatarini;
- (d) Kufuata taratibu bora za kisheria, kiufundi, kiutawala na kifedha kwa lengo la:
  - (i) kuendeleza uundaji au uimarishaji wa asasi ili kutoa mafunzo ya usimamizi wa turathi za tamaduni zisizogusika na kusambazika kwa turathi hizo kupitia kwa vikao na maeneo yaliyopangiliwa kufanyiwa maonyesho au mwoneko wa namna fulani;
  - (ii) kuhakikisha kufikiwa kwa turathi za tamaduni zisizogusika huku desturi za kitamaduni zinazosimamia baadhi ya vipengee vya turathi hizo zikiheshimiwa vilivyo;
  - (iii) kuanzisha asasi za kuhifadhi nyaraka kuhusu turathi za tamaduni zisizogusika na kuwezesha nyaraka hizo kufikiwa.

### **Kifungu cha 14 – Elimu, Uhamasishaji na Uimarishaji Mafunzo**

Kwa kila njia inayofaa, kila Taifa Mwanachama:

- (a) Litahakikisha, utambuaji wa, kuheshimiwa kwa, na ukuboresha wa turathi za tamaduni zisizogusika katika jamii, hususan kupitia kwa:

- (i) elimu, uhamasishaji na mipango ya mawasiliano, inayolenga umma, hususan vijana;
- (ii) miradi maalum ya elimu na mafunzo katika jamii na makundi husika;
- (iii) shughuli za uimarishaji wa mafunzo zinazohusiana na ulinzi wa turathi za tamaduni zisizogusika, hususan usimamizi na utafiti wa kisayansi; na
- (iv) njia zisizo rasmi za kusambaza maarifa;

(b) kufahamisha umma kuhusu vitu vinavyoathiri vibaya turathi hizo na shughuli zinazoendeshwa ili kuyafuatilia Maafikiano hayo;

(c) kuendeleza elimu inayohusiana na ulinzi wa maeneo ya kiasili na ukumbusho ambayo kuwepo kwake ni muhimu katika kuzifafanua turathi za tamaduni zisizogusika.

#### **Kifungu cha 15 – Ushiriki wa Wanajamii, Vikundi na Watu binafsi**

Kuambatana na mfumo wa shughuli za kulinda turathi za tamaduni zisizogusika, kila Taifa Mwanachama litajitahidi kuwa na ushiriki wa jamii nyingi, vikundi na, ikiwa inafaa, watu wanaounda, kusimamia na kuendesha turathi hizo ili kuwahusisha vilivyo katika usimamizi wake.

### **IV. Kulinda turathi za tamaduni zisizogusika katika kiwango cha kimataifa**

#### **Kifungu cha 16 – Orodha ya Uwakilishi ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Kibinadamu**

1. Ili kuhakikisha kwamba pana mwoneko bora kuhusu turathi za tamaduni zisizogusika, kufahamika kwa umuhimu wake na kushinikiza mazungumzo kuhusu uanuwai wa kitamaduni, kwa kuzingatia mapendekezo ya Mataifa Wanachama husika, Kamati hiyo itaanzisha, kudumisha na kuchapisha Orodha Wakilishi ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Kibinadamu kila wakati.

2. Kamati hiyo itatayarisha mapendekezo na kuyawasilisha kwa Mkutano Mkuu kwa lengo la kuidhinisha vigezo vya kuanzisha, kurekebisha na kuchapisha hii Orodha Wakilishi.

#### **Kifungu cha 17 – Orodha ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika zinazohitaji ulinzi wa dharura**

1. Kwa lengo la kuchukua hatua zinazofaa za kiulinzi, Kamati hiyo itabuni, kuiweka vyema na kuichapisha Orodha ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika zinazohitaji ulinzi wa haraka, na itaandikisha turathi kama hiyo kwenye orodha kwa kufuatia ombi na Taifa Mwanachama husika.

2. Kamati hiyo itatayarisha mapendekezo na kuyawasilisha kwa Mkutano Mkuu kwa lengo la kuidhinisha vigezo vya kuanzisha, kurekebisha, na hali kadhalika kuichapisha.

3. Katika hali ya dharura kubwa – kigezo kisichoegemea upande wowote ambacho kitaidhinishwa na Mkutano Mkuu kupitia kwa ombi la Kamati – Kamati hiyo inaweza kuandikisha faridi moja ya turathi husika kwenye orodha ya uwakilishi kama ilivyotajwa kwenye aya ya 1, kwa ushauri wa Taifa Mwanachama husika.



### **Kifungu cha 18 – Mipango, miradi na shughuli za kulinda turathi za tamaduni zisizogusika**

1. Kwa mujibu wa mapendekezo yaliyowasilishwa na Mataifa Wanachama, na kulingana na vigezo vitakavyofafanuliwa na Kamati pamoja na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu, kila baada ya kipindi fulani Kamati itachagua na kuchangia katika miradi na shughuli, ukuzaji wa mipango ya kitaifa, kijimbo na kieneo ili kuhifadhi turathi ambazo inafikiria kuwa muhimu katika kuangazia maadili na malengo ya Mkataba, huku ikizingatia yale mahitaji maalumu ya nchi zinazostawi.
2. Kufuatia masuala haya, Kamati itapokea, kuchunguza na kuidhinisha maombi ya usaidizi wa kimataifa kutoka kwa Mataifa Wanachama ili kutayarisha mapendekezo hayo.
3. Kamati itaambatanisha utekelezwaji wa miradi, mipango na shughuli kama hizi kupitia usambazaji wa njia bora za kuzingatiwa kwa kutumia mbinu itakazoamua yenyewe.

## **V. Ushirikiano na Usaidizi wa Kimataifa**

### **Kifungu cha 19 – Ushirikiano**

1. Kwa mujibu wa Maafikiano haya, ushirikiano wa kimataifa unahusisha ubadilishanaji wa habari na tajriba, ari za pamoja na kuanzishwa kwa njia muafaka za kusaidia Mataifa Wanachama katika harakati zao za kuhifadhi turathi za tamaduni zisizogusika, miongoni mwa mengine.
2. Bila kuathiri utaratibu wa vifungu vya sheria za taifa, zikiwemo pia sheria za mila na desturi, Mataifa Wanachama yanatambua kwamba Ulinzi wa Turathi za Tamaduni Zisizogusika ni muhimu kwa binadamu, na kutokana na hili, yamejitolea kushirikiana katika viwango vya nchi moja na nyingine, kieneo, ki-kanda na kimataifa.

### **Kifungu cha 20 – Sababu za Usaidizi wa Kimataifa**

Usaidizi wa Kimataifa unaweza kutolewa kwa sababu zifuatazo:

- (a) Kuhifadhi turathi zilizoandikwa kwenye Orodha ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika Zinazohitaji Ulinzi wa dharura;
- (b) Utayarishaji wa orodha ya turathi zisizogusika kulingana na Kifungu cha 11 na 12;
- (c) Usaidizi wa mipango, miradi na shughuli zinazotekelezwa katika viwango vya taifa, kieneo na ki-kanda, unaolenga kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika;
- (d) Sababu nyingine yoyote ambayo Kamati itafikiria kuwa muhimu.

### **Kifungu cha 21 – Njia za Usaidizi wa Kimataifa**

Usaidizi utakaotolewa na Kamati kwa Mataifa Wanachama utatawaliwa na maelekezo ya kiutendakazi kama yanavyobainika katika Kanuni ya 7 na katika maafikiano yanayorejelewa kwenye Kifungu cha 24, na ambayo yanaweza kujitokeza kwa njia zifuatayo:

- (a) Uchunguzi wa vipengele mbali mbali vya ulinzi;

- (b) Kutoa wataalamu na wajuzi wa kazi mbali mbali;
- (c) Kutoa mafunzo kwa wafanyi kazi wanaohitajika;
- (d) Upanuzi wa mbinu za ubora wa kazi na vipimo vinginevyo;
- (e) Uundaji na utekelezaji wa miundo msingi;
- (f) Utoaji wa vifaa na ujuzi;
- (g) Njia zinginezo za usaidizi wa kifedha na kiufundi, ikiwepo utoaji wa mikopo yenye viwango vya chini vya riba, pamoja na michango.

### **Kifungu cha 22 – Masharti yanayoongoza Usaidizi wa Kimataifa**

1. Kamati itaandaa utaratibu wa kuchunguza maombi ya usaidizi wa kimataifa, na itaeleza bayana habari zitakazojumuishwa katika maombi hayo kama vile hatua zinazotazamiwa kuchukuliwa, mbinu zinazohitajika pamoja na makadirio ya gharama.
2. Pakiwa na dharura, maombi ya usaidizi yatachunguzwa na kupewa kipaumbele na Kamati.
3. Ili kufikia uamuzi, Kamati itachukua hatua za kuchunguza na kufanya mashauriano kwa kadri itakavyohitajika.

### **Kifungu cha 23 – Maombi ya Usaidizi wa Kimataifa**

1. Kila Taifa Mwanachama linaweza kutuma ombi la usaidizi wa kimataifa kwa Kamati kwa minajili ya kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika zilizo katika mipaka ya eneo lake.
2. Ombi kama hilo linaweza pia kuwasilishwa kwa pamoja na Mataifa Wanachama mawili au zaidi.
3. Ombi hilo litahusisha masharti yaliyomo katika Kifungu cha 22 aya ya 1, zikiwepo nyaraka zote muhimu.

### **Kifungu cha 24 – Jukumu la Mataifa Wanachama yatakayonufaika**

1. Kuambatana na vifungu vya Makubaliano haya, usaidizi wa kimataifa unaotolewa utadhibitiwa kupitia kwa makubaliano baina ya Kamati na Taifa Mwanachama litakalonufaika.
2. Kama kanuni ya jumla, Taifa Mwanachama linalonufaika kutokana na usaidizi wa kimataifa halina budi kuchangia katika kugharamia hatua za kulinda tamaduni hizo kulingana na uwezo wake wa kirasilmali.
3. Taifa Mwanachama linalonufaika kutokana na usaidizi litawasilisha kwa kamati ripoti kuhusu matumizi ya usaidizi uliotolewa kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika.

## VI. Hazina ya Turathi za Kulinda Tamaduni Zisizogusika

### Kifungu cha 25 – Muundo na Rasilmali za Hazina

1. “Hazina ya Kulinda Turathi za Tamaduni Zisizogusika” ambayo hapa itajulikana kama “Hazina” imeanzishwa.
2. Hazina itahusisha hazina-mdhamana kulingana na Taratibu za Kifedha za UNESCO.
3. Rasilmali ya Hazina itahusisha:
  - (a) Michango itakayotolewa na Mataifa Wanachama;
  - (b) Fedha zilizotengwa na Baraza Kuu la UNESCO kwa malengo haya;
  - (c) Michango, zawadi au mirathi ambayo huweza kutolewa na:
    - (i) Mataifa mengine;
    - (ii) Mashirika na programu za Utaratibu wa Umoja wa Mataifa hususan, Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo (*UNDP*), pamoja na mashirika mengine ya kimataifa;
    - (iii) Mashirika ya umma, ya kibinafsi, au watu binafsi;
  - (d) Riba yoyote inayotokana na rasilmali ya Hazina;
  - (e) Fedha zinazotokana na michango, yakiwemo pia malipo yanayotokana na shughuli zinazotekelezwa kwa manufaa ya Hazina hiyo;
  - (f) Rasilmali nyingine yoyote inayotokana na kanuni za Hazina zitakazoandikwa na Kamati.
4. Matumizi ya rasilmali na Kamati yataamuliwa kulingana na misingi ya mwongozo uliowekwa na Mkutano Mkuu.
5. Kamati inaweza kukubali michango pamoja na aina yoyote ya misaada kwa malengo ya jumla na mahsusi ya miradi maalumu, ilimradi miradi hiyo iwe imeidhinishwa na Kamati.
6. Hakuna masharti yoyote ya kisiasa, kiuchumi au mengineyo yasiyoambatana na malengo ya Maafikiano haya, ambayo yanaweza kuhusishwa na michango inayotolewa kwa Hazina.

### Kifungu cha 26 – Michango ya Mataifa Wanachama kwa Hazina

1. Bila kuwa na upendeleo kwa michango yoyote ya ziada inayotolewa kwa hiari, katika Maafikiano haya, Mataifa Wanachama yatawajibika kutoa malipo kwa Hazina angalau kila baada ya miaka miwili, na kiasi cha michango ambayo itakuwa asilimia sawa na ile itakayotolewa na Mataifa yote, na ambayo itaamuliwa katika Mkutano Mkuu. Uamuzi huo wa Mkutano Mkuu utatolewa na idadi iliyo kubwa ya Mataifa Wanachama yatakayokuwepo kupiga kura, na ambayo hayatakuwa yametoa azimio linalorejelewa katika aya ya 2 ya Kifungu hiki. Hakuna wakati ambapo mchango wa Taifa Mwanachama utazidi 1% ya mchango wake wa kawaida kwa bajeti ya UNESCO.

2. Hata hivyo, kila Taifa linalorejelewa kwenye Kifungu cha 32 au 33 cha Maafikiano haya linaweza kutangaza wakati wa kuweka vyombo vyake vya kuidhinisha rasmi, kukubali, kuthibitisha au kupitisha, kwamba halitafungwa na mahitaji ya aya 1 ya Kifungu hiki.

3. Taifa Mwanachama katika Maafikiano haya ambayo yametoa maamuzi yanayorejelewa kwenye aya 2 ya Kifungu hiki kinaweza kufutilia mbali maamuzi hayo kwa kumjulisha Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO. Hata hivyo, kuondolewa kwa maamuzi hayo hakutawezekana iwapo kuna mchango ambao Taifa husika linahitaji kutoa, hadi pale tarehe ya kikao kingine cha Mkutano Mkuu kitakapoitishwa.

4. Ili kuiwezesha Kamati kuratibisha mikakati yake vizuri, michango ya Mataifa Wanachama katika Maafikiano haya ambayo yametoa maamuzi yanayorejelewa kwenye aya 2 ya Kifungu hiki, italipwa kwa wakati, angalau kila baada ya miaka miwili, kiasi kinachokaribiana sana na michango ambayo yangedaiwa kama yangehitajika kulipa kufuatia sheria ya aya ya 1 kwenye Kifungu hiki.

5. Taifa Mwanachama lolote, katika Maafikiano haya ambayo yana malimbikizi ya malipo ya lazima ama ya hiari katika mwaka uliopo na ule ulioutangulia hivi karibuni, halitaweza kuwa Mwanachama wa Kamati; Sharti hili halitahusu uchaguzi wa kwanza. Kipindi cha kuwa ofisini kwa Taifa lolote kama hilo ambalo tayari ni Mwanachama wa Kamati, kitakwisha wakati wa uchaguzi kulingana na Kifungu cha 6 ya Maafikiano hayo.

#### **Kifungu cha 27 – Michango ya hiari na ziada kwa Hazina**

Mataifa Wanachama ambayo yangependa kutoa michango ya hiari zaidi ya ile inayofafanuliwa katika Kifungu cha 26 yataweza kuifahamisha Kamati haraka iwezekanavyo ili kuiwezesha kupanga mikakati yake ipasavyo.

#### **Kifungu cha 28 – Kampeni za Kimataifa za Kuchangisha fedha**

Mataifa Wanachama, pakiwa na uwezekano, yataanzisha kampeni za kimataifa za kusaidia kuchanga fedha zitakazokusanywa kwa manufaa ya Hazina chini ya usaidizi wa UNESCO.

### **VII. Ripoti**

#### **Kifungu cha 29 – Ripoti za Mataifa Wanachama**

Mataifa Wanachama yatawasilisha kwa Kamati, yakizingatia maumbo na nyakati zilizobainishwa na Kamati, ripoti kuhusu hatua za kisheria, kanuni na hatua nyinginezo zilizochukuliwa kuwezesha utekelezwaji wa Maafikiano haya.

#### **Kifungu cha 30 – Ripoti za Kamati**

1. Kwa misingi ya shughuli zake pamoja na ripoti za Mataifa Wanachama zilizorejelewa kwenye Kifungu cha 29, Kamati itawasilisha ripoti kwenye Mkutano Mkuu katika kila mojawapo ya vikao vyake.

2. Ripoti hiyo itawasilishwa kwa Kongamano Kuu la UNESCO.

### **VIII. Ibara ya Mpito**

#### **Kifungu cha 31 – Uhusiano wa Tamko Rasmi la Vito vya Masimulizi na Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Binadamu**

1. Kamati itahusisha vitu vyote vilivyotangazwa “Vito vya Masimulizi na Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Ubinadamu” kabla ya kuanzishwa kwa Maafikiano haya katika Orodha Wakilishi ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Binadamu.
2. Kujumuishwa kwa vitu hivi kwenye Orodha Wakilishi ya Turathi za Tamaduni Zisizogusika za Ubinadamu hakutakata hukumu kiawali ili kutothamini vigezo vitakavyozingatiwa baadaye katika maandiko ya ukumbusho yatakayoafikiwa kulingana na Kifungu cha 16 aya ya 2.
3. Hakuna Tamko rasmi lolote litakalotolewa baada ya kuanzishwa kwa Maafikiano haya.

### **IX. Ibara za Mwisho**

#### **Kifungu cha 32 – Kuidhinishwa, Kukubalika au Kupitishwa**

1. Maafikiano haya yatategemea uidhinisho, ukubalifu na kupitishwa na Mataifa Wanachama wa UNESCO kulingana na taratibu za katiba zao.
2. Vyombo vya kuidhinisha, kukubali au kupitishwa vitawekwa katika hifadhi ya Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO.

#### **Kifungu cha 33 – Ukubalifu**

1. Maafikiano yatakuwa wazi kukubaliwa na Mataifa yote yasiyo Wanachama wa UNESCO, ambayo yamealikwa na Kongamano Kuu la UNESCO kuyakubali.
2. Maafikiano haya pia yatakuwa wazi kukubaliwa na nchi zinazofurahia serikali ya ndani inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa, lakini ambazo hazijapata uhuru kamili kulingana na azimio la 1514 (XV) la Baraza Kuu, na zinaelewa masharti yanayotawala Maafikiano haya ukiwemo umilisi kuhusiana na masuala yanayosimamiwa na Maafikiano haya, ukiwepo umilisi wa kujihusisha na mapatano yanayoambatana na masuala haya.
3. Chombo cha ukubalifu kitawekwa katika hifadhi ya Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO.

#### **Kifungu cha 34 – Utekelezwaji**

Maafikiano haya yaanza kutekelezwa miezi mitatu baada ya tarehe ya kuwekwa kwa chombo cha thelathini cha kuidhinisha, kukubalika, kupitishwa au ukubalifu, lakini ni yale Mataifa tu ambayo yameweka vyombo vyao vya kuidhinisha, kukubali, kupitishwa au ukubalifu katika au kabla ya

siku hiyo. Maafikiano hayo yaanza kutekelezwa kwa Taifa Mwanachama lolote, miezi mitatu baada ya kuweka vyombo vya kuidhinisha, kukubali, kupitisha au ukubalifu.

### **Kifungu cha 35 – Mifumo ya Serikali za Shirikisho au Serikali zisizo na mfumo mmoja wa kiutawala**

Masharti yafuatayo yatahusisha Mataifa Wanachama yaliyo na mifumo ya serikali za shirikisho au serikali zisizo na mfumo mmoja wa kiutawala:

(a) Kwa mujibu wa masharti ya Maafikiano haya ambayo utekelezaji wake upo chini ya mfumo wa serikali ya shirikisho au chini ya nguvu za sheria kuu, kuwajibika kwa serikali ya shirikisho au serikali kuu kutakuwa sawa kama kuwajibika kwa Mataifa Wanachama yasiyo ya shirikisho;

(b) Kwa mujibu wa kanuni za Maafikiano haya, utekelezwaji wake ambao upo chini ya mamlaka ya Mataifa, nchi, mikoa au majimbo binafsi ambayo hayalazimishwi na utaratibu wa sheria za ushirikisho kuchukua hatua za kisheria, serikali ya shirikisho itafahamisha halmashauri bora za mataifa, nchi, mikoa na majimbo kama hayo kuhusu kanuni hizo, pamoja na mapendekezo yake ya uidhinishaji.

### **Kifungu cha 36 – Kujiondoa kwenye Maafikiano**

1. Kila Taifa Mwanachama linaweza kujiondoa kwenye Maafikiano haya.
2. Kujiondoa huku kutafanywa kwa kuandika barua itakayopelekwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO.
3. Kujiondoa huku kutatekelezwa katika kipindi cha miezi kumi na miwili baada ya barua hiyo kupokelewa. Kujiondoa huku hakutaathiri kwa vyovyote vile uwajibikaji wa kifedha wa Taifa Mwanachama linalojiondoa, mpaka tarehe ya kujiondoa huko itakapotimia.

### **Kifungu cha 37 – Majukumu ya Uwekaji**

Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO, kama Kiongozi wa Uwekaji wa Maafikiano, atayafahamisha Mataifa Wanachama wa Shirika, nchi ambazo si wanachama wa Shirika hilo kama zilivyotajwa katika Kifungu cha 33, na pia katika Umoja wa Mataifa kuhusu uwekaji wa vyombo vyote husika vya uidhinishaji, kukubali, upitishaji na ukubalifu kama ilivyowekwa kwenye Kifungu cha 32 na 33, na kujiondoa kwenye Maafikiano kama ilivyowekwa katika Kifungu cha 36.

### **Kifungu cha 38 – Marekebisho**

1. Taifa Mwanachama linaweza kupendekeza marekebisho ya Maafikiano haya kwa kumwandikia Mkurugenzi Mkuu. Mkurugenzi Mkuu atasambaza mawasiliano haya kwa Mataifa yote Wanachama. Iwapo kwenye kipindi cha miezi sita tokea tarehe ambayo mawasiliano hayo yalisambazwa siyo Mataifa Wanachama chini ya nusu yatakuwa yamejibu kikamilifu kulikubalia ombi hilo, Mkurugenzi Mkuu atawasilisha pendekezo hilo katika kikao kijacho cha Kongamano Kuu ili kujadiliwa na kuweza kukubaliwa.

2. Marekebisho yatakubaliwa na thuluthi mbili ya Mataifa Wanachama yaliyohudhuria na kupiga kura.

3. Baada ya kukubalika, marekebisho ya Mkataba huo yatatolewa ili kuidhinishwa, kukubalika, kupitishwa au ukubalifu wa Mataifa Wanachama.

4. Marekebisho yataanza kutekelezwa ila tu kwa yale Mataifa Wanachama ambayo yatakuwa yameidhinisha, kukubali, kupitisha au ukubalifu wayo miezi mitatu baada ya uwekaji wa vyombo hivyo vinavyorejelewa katika aya ya 3 ya Kifungu hiki, na kupitia thuluthi mbili ya Mataifa Wanachama. Baada ya hapo, kila Taifa Mwanachama linaloidhinisha, kukubali, kupitisha au kurekebisha, marekebisho hayo yataanza kutekelezwa miezi mitatu baada ya tarehe ya Taifa hilo Mwanachama kuweka vyombo vyake vya kuidhinisha, kukubali, kupitisha au upatikanaji wavyo.

5. Utaratibu ulioelezwa katika aya ya 3 na 4 hautazingatiwa katika marekebisho ya Kifungu cha 5 kuhusu idadi ya Mataifa Wanachama katika Kamati. Marekebisho yataanza kutekelezwa wakati yatakapokubaliwa.

6. Taifa litakalokuwa Mwanachama wa Maafikiano haya baada ya marekebisho kuanza kutekelezwa kulingana na aya ya 4 ya Kifungu hiki kitaweza kutofikisha ujumbe tofauti uliotazamiwa, ili ujumbe huo uhusishwe:

(a) kama Mwanachama wa Maafikiano haya kama yalivyorekebisha; na

(b) kama Mwanachama wa Maafikiano ambayo hayakurekebisha, na kama Taifa Mwanachama lolote lisilofungamanishwa na marekebisho hayo.

### **Kifungu cha 39 – Matini za Kuaminika**

Maafikiano haya yametolewa kwa Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kirusi na Kihispania, matini zote sita zikiwa za kuaminika.

### **Kifungu cha 40 – Usajili**

Kulingana na ilivyo Kifungu cha 102 cha Mapatano ya Umoja wa Mataifa, Maafikiano haya yatasajiliwa katika Afisi ya Umoja wa Mataifa kupitia kwa ombi la Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO.